

Tunathibitisha viyi kuwa Yule Malaika wa (Yohana 5:4) ni wa  
MUNGU?

**Swali:** Je! tunaweza kuthibitisha viyi kuwa Yule malaika aliyejewa  
anashuka na kuyatibua maji alikuwa ni malaika wa MUNGU na si wa  
shetani, kwasababu maandiko yanasema kuwa shetani naye anaweza  
kujigeuza na kuwa mfano wa malaika wa nuru (*2Wakorintho 11:14*).

**JIbu:** Turejee..

*Yohana 5:1 “Baada ya hayo palikuwa na sikukuu ya Wayahudi; naye Yesu akakwea kwenda Yerusalem. 2 Na huko Yerusalem penye mlango wa kondoo pana birika, iitwayo kwa Kiebrania Bethzatha, nayo ina matao matano.*

*3 Ndani ya hayo jamii kubwa ya wagonjwa walikuwa wamelala, vipofu, viwete, nao waliopooza, [wakingoja maji yachemke.*

*4 Kwa maana kuna wakati ambapo MALAIKA HUSHUKA, AKAINGIA KATIKA ILE BIRIKA, AKAYATIBUA MAJI. Basi yeye aliyeingia wa kwanza baada ya maji kutibiliwa, AKAPONA UGONJWA WOTE ULIOKUWA UMEMPATA.]”*

Ni kweli Biblia inasema shetani anaweza kujigeuza na kuwa mfano wa Malaika wa Nuru, lakini haisemi kuwa anaweza kujigeuza na kuwa

Tunathibitisha vipi kuwa Yule Malaika wa (Yohana 5:4) ni wa  
MUNGU?

Malaika wa Nuru, bali mfano wa..

Kwahiyo huyu tunayemsoma hapa katika Yohana 5:4 hakuwa malaika wa giza, kwasababu matunda yake si ya giza kwani Maandiko yanasema “shetani hawezi kumtoa shetani mwenzake”.

*Mathayo 12:25 “Basi Yesu akijua mawazo yao, akawaambia, Kila ufalme ukifitinika juu ya nafsi yake, hufanyika ukiwa; tena mji au nyumba yo yote ikifitinika juu ya nafsi yake, haitasimama.*

*26 Na SHETANI AKIMTOA SHETANI, AMEFITINIKA JUU YA NAFSI YAKE; basi ufalme wake utasimamaje?”*

Sasa wote waliokuwa wamelala pale walikuwa wanasumbuliwa na magonjwa yaliyoletwa na mapepo, kwasababu asilimia kubwa ya magonjwa yanababishwa na mapepo (*soma Mathayo 9:32 na Mathayo 12:22*).

Sasa kwa mantiki hiyo haiwezekani malaika wa giza kushuka na kuwatoa malaika wenzake wa giza (*yaani mapepo*) wenzao ndani ya watu, ni jambo ambalo haliwezekani!, vinginevyo ufalme wa giza

Tunathibitisha vipi kuwa Yule Malaika wa (Yohana 5:4) ni wa  
MUNGU?

usingesimama, kwahiyio Yule malaika alikuwa anashuka kuyatibua maji  
ni malaika wa Nuru na si wa giza.

Jambo la ziada la kujifunza ni kwamba watu wanaokwenda kwa  
waganga wa kienyeji kwaajili ya kutatuliwa shida zao au magonjwa yao  
na baada ya kupiga ramli wanaona kama wamepona..

Kiuhalisia ni kwamba hawajatatuliwa matatizo yao bali ndio  
yameongezwa, kwamfano mtu ataenda kwa mganga akiwa na tatizo la  
homa, na anaaguliwa na kujiona amepona kabisa, na kuambiwa kuwa  
majini yamefukuzwa ndani yake.

Sasa kiuhalisia kulingana na biblia yale mapepo hayajaondoka!, bali  
yamehamishwa kutoka sehemu moja ya mwili kwenda nyingine, au  
kutoka sehemu moja ya maisha kwenda nyingine, lakini si kwamba  
**yamefukuzwa/kuondolewa** kabisa kutoka katika maisha yake,

Maana yake sasa huyu mtu atapata unafuu kwenye kifua kilichokuwa  
kinamshumbua, au kwenye mguu, lakini lile pepo limehamia kwenye  
tumbo, au miguu, au limepelekwa kusababisha matatizo mengine katika  
maisha ya Yule mtu, na tena mtu anayeenda kwa mganga anakuwa  
anaongezewa mapepo mengine kwa ajili ya matatizo mengine  
yatakayotokea wakati huo huo au wakati mwingine huko mbeleni,

Tunathibitisha vipi kuwa Yule Malaika wa (Yohana 5:4) ni wa  
MUNGU?

kwasababu shetani kamwe hawezi kumtoa shetani mwenzake.

Bwana akubariki.

Washirikishe na wengine habari hizi njema kwa kushea

Ikiwa utapenda kupata msaada wa kumpokea Yesu maishani mwako  
bure, Basi wasiliana nasi kwa namba uzionazo chini ya makala hii.

Pia kwa kupokea mafundisho ya kila siku kwa njia ya WHATSAPP, jiunge  
na channel yetu kwa kubofya link hii >>

**<https://whatsapp.com/channel/0029VaBVhuA3WHTbKoz8jx10>**

Kwa mawasiliano: +255693036618 au +255789001312

Bwana akubariki.

**Mafundisho mengine:**

**BIRIKA LA SILOAMU.**

**[Birika ni nini?, na yale Matao matano katika birika la Bethzatha](#)**

Tunathibitisha vipi kuwa Yule Malaika wa (Yohana 5:4) ni wa  
MUNGU?

**ni nini?.**

**JE BADO UNASUBIRIA MAJI YACHEMKE?**

**AKAWAPONYA WALE WENYE HAJA YA KUPONYWA**

**WAKO WATATU WASHUHUDIAO MBINGUNI NA DUNIANI.**

Share on:

WhatsApp